# KWA NINI AGANO LA KALE LILISHINDWA

**JOE CREWS**

# KWA NINI AGANO LA KALE LILISHINDWA

**Na Joe Crews**

(Hotuba Na. 13 ya Mambo ya Kweli Yanayoshangaza)

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Why the Old Covenant Failed - Kiswahili

# Kwa Nini Agano la Kale Lilishindwa

Wakati fulani uliopita mimi nilitoka kwenye jukwaa mwisho wa ujumbe wa injili, na kuharakisha kwenda kwenye mlango wa mbele kuwasalimu watu. Ghafula njia yangu ikazuiwa na vijana wa kiume watatu, mmoja wao alizungumza nami kwa sauti kubwa sana. Alisema, "Ndugu Joe, tulivunjwa moyo kwa njia uliyotumia kutuweka sisi chini ya Agano la Kale usiku huu wa leo kwa kuhubiri juu ya Sabato ya siku ya saba [Jumamosi]. Je, wewe hutambui kwamba sisi tunaishi chini ya Agano Jipya sasa, na kwamba ingetupasa kuitunza Jumapili [siku ya kwanza ya juma] badala ya hiyo Sabato [Jumamosi]?"

Kijana yule mwanaume alikuwa anasema maneno yanayoiwakilisha imani ya maelfu mengi ya Wakristo wa siku hizi, ambao kwa moyo mnyofu wanaamini kwamba Amri Kumi zilikuwa ndilo lile Agano la Kale ambalo lilitokomea pale msalabani, na kwa hiyo hazitumiki kwa wakati huu kwa Wakristo waliookolewa kwa neema. Je, hiyo ni hoja ya kweli? Kama ni ya kweli, basi, kwa hakika yunayo haja ya kuambiwa juu ya fundisho hilo ili kuepuka kuanguka katika shimo la kufisha la wokovu kwa njia ya Sheria (legalism). Kwa upande mwingine, lingekuwa ni kosa la kufisha mno kuipunguza hata moja katika amri zile kuu [kumi] za maadili.

Hakuna awezaye kukana kwamba kuna semi nyingi za [Vitabu vya] Agano la Kale zinazotaja Amri Kumi kama agano; walakini litakuwa ni kusudi letu hapa kuonyesha ya kwamba Sheria ile ya amri Kumi HAIKUWA Agano lile la Kale ambalo liliondolewa.

Lakini kabla hatujalichimba sana somo hili linalosisimua, hatuna budi kufafanua agano (covenant) ni kitu gani hasa? Zipo aina nyingi [za maagano] na mifumo yake, lakini kimsingi *agano ni mapatano kati ya pande mbili ambayo yamejengwa juu ya ahadi zinazokubalika pande zote mbili*. Kupitia katika karne zote Mungu ameshughulika na watu wake kwa msingi wa maagano. Ni Mungu mwenye busara, naye anatualika, anasema, "Haya, njoni, tusemezane." Isaya 1:18.

Wakati mwingine Mungu alianzisha mapatano (pacts) na mtu mmoja mmoja kama vile Musa, Ibrahimu, na Daudi, na wakati mwingine pamoja na taifa la Israeli. Agano lililo la maana kuliko yote lilianzishwa muda mrefu kabla ya kuumbwa dunia hii. Lilikuwa ni agano kati ya Baba na Mwana, nalo lilihusika na kuondolewa kwa dhambi hatimaye. Yesu alijitolea mwenyewe kule juu kama "Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia" (Ufu. 13:8) katika ule umilele mpana mno wa zama zile zilizopita. Alikubali kuwa sadaka ya upatanisho ili kumkomboa mwanadamu, endapo Adamu na hawa wangechagua kutenda dhambi.

Masharti ya agano lile la milele hayajapata kubadilishwa kamwe au kubatilishwa [kufutwa]. Ijapokuwa maagano mengine mengi yameanzishwa kupitia katika miaka mingi, mpango rahisi wa wokovu kwa njia ya imani umeendelea kuwa na nguvu katika vizazi vyote, kwa wanadamu wote.

Hata hivyo, agano ambalo limeleta kutokuelewana kwingi sana, linaitwa na mwandishi yule wa kitabu cha Waebrania kuwa ni "Agano la Kale" (Old Covenant – Mapatano ya Kale; sio vitabu vile vya Agano la Kale kuanzia Mwanzo hadi Malaki). Pia anaeleza kuwekwa kwa Agano Jipya (New Covenant – Mapatano Mapya; sio vitabu vya Agano Jipya kuanzia Mathayo hadi Ufunuo) ambalo kwa kadiri fulani lina manufaa ya maana sana kuliko lile la kale. Hapa ni namna anavyoyaeleza yote mawili. "Lakini sasa amepata huduma iliyo bora zaidi, kwa kadiri alivyo mjumbe wa agano lililo bora, lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora. Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili. Maana, awalaumupo, asema, Angalia, siku zinakuja, asema Bwana,

Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda *agano jipya*; halitakuwa kama agano lile nililoagana na baba zao, katika siku ile nilipowashika mikono yao niwatoe katika nchi ya Misri. Kwa sababu hawakudumu katika agano langu, Mimi nami sikuwajali, asema Bwana. Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Israeli baada ya siku zile, asema Bwana, *Nitawapa sheria* [amri kumi] *zangu katika nia zao, katika mioyo yao nitaziandika*; Nami nitakuwa Mungu kwao, nao watakuwa watu wangu…. Kwa sababu *nitawasamehe maovu yao*, na *dhambi zao sitazikumbuka tena*. Kwa kule kusema *Agano Jipya*, amelifanya lile la kwanza [la kale] kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzapo kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka." Waebrania 8:6-13.

Maelezo hayo hayaachi nafasi yo yote ya mashaka kuhusu ajali ya Agano la Kale. Liliwekwa kando kwa kulipendelea lile jipya ambalo lilikuwa na ahadi bora. Kwa kawaida, tunapenda kujua yote juu ya agano lile jipya ambalo litatia Sheria ya Mungu [Amri Kumi – Kut. 20:3-17] moyoni na katika nia. Lakini pia tunahitaji kuelewa asili ya agano lile lililotoweka. Mamilioni ya watu wamefundishwa kwamba agano lile lilikuwa ni ile Sheria ya Amri Kumi. Wanajigamba kwamba wamekombolewa kutoka katika sheria hiyo [Amri Kumi], tena wanadai kwamba wanatembea katika uhuru wenye utukufu mbali na agano lile la matendo la kitabu cha Agano la Kale.

## Agano la Kale Sio Zile Amri Kumi

Je, huo ni msimamo wa Biblia? Ni muhimu vile vile kujua Agano la Kale kile ambacho halikuwa, kama ilivyo kujua kile ambacho lilikuwa. Sasa hivi hebu na tuangalie ushahidi kamili wa aina tatu unaoonyesha kwamba agano lile lililotoweka halikuwa zile Amri Kumi. Kisha tutaamua kwa kulinganisha andiko kwa andiko kuona Agano la kale lilikuwa ni kitu gani hasa.

Kwanza kabisa, tunaona ya kwamba Agano la Kale lilikuwa na baadhi ya ahadi hafifu ndani yake. Agano Jipya, tunaambiwa, "lililoamriwa juu ya ahadi zilizo bora." Fungu la 6. Hebu niambieni basi, je! mtu ye yote wakati wo wote uliopita ameweza kuonyesha ahadi yo yote iliyo hafifu katika zile Amri Kumi? Hasha. Kinyume chake, Paulo anatangaza kwamba zilikuwa njema sana [Rum. 7:12,13]. "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate uheri, ukae siku nyingi katika dunia." Waefeso 6:1-3.

Tangazo hilo peke yake latosha kuonyesha kwamba mwandishi wa kitabu cha Waebrania alikuwa haishtaki Sheria ile ya Maadili [Amri Kumi] kuwa ina ahadi zilizo hafifu. Agano la Kale, hata kama lingekuwa ni kitu kingine kiwacho chote kile, kamwe halingeweza kuwa zile Amri Kumi.

Jambo la pili lililokwenda kombo kuhusu lile Agano la Kale ni kwamba lilikuwa na upungufu. Biblia yasema hivi: "Maana kama lile la kwanza lingalikuwa halina upungufu, nafasi isingalitafutwa kwa lile la pili." Waebrania 8:7. Hebu na niwaulize swali: Je, kuna mtu ye yote ambaye kwa wakati wo wote ule ameweza kuona upungufu au kosa katika maandishi yale yaliyoandikwa kwa mkono wa Mungu [Kut. 31:18]? Mtunga Zaburi alitangaza, alisema, "Sheria ya Bwana [Amri Kumi] ni kamilifu, huiburudisha nafsi." Zaburi 19:7. Paulo aliandika hivi: "Basi torati [sheria/Amri Kumi] ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema." Warumi 7:12.

Je! maneno hayo yanasikika kana kwamba yanataja kitu fulani kilicho dhaifu na kisicho kikamilifu? Hakuna sheria iwayo yote ambayo ingeweza kuwa kamilifu na kuwa na upungufu wakati ule ule. Inakuwa dhahiri zaidi na zaidi kwamba Agano la Kale lisingeweza kuwa zile Amri Kumi.

Mwisho, hata hivyo, twasoma jambo la kuvutia mno juu ya lile Agano la Kale - lilikusudiwa kuondolewa! "Kwa kule kusema, Agano Jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka." Waebrania 8:13. Basi, tunaweza kuuliza swali zito ambalo lingemaliza kila shaka juu ya jambo hili. Je! Sheria ile Kuu ya Maadili ya

Amri Kumi ilitoweka? Mtu ye yote aliyesoma [vitabu vya] Agano Jipya hana budi kujibu, La, Hasha. Paulo kwa uthabiti anasema kinyume kabisa kwa habari ya Sheria hiyo [Amri Kumi]. Aliuliza swali hili, "Basi, je! twaibatilisha Sheria [Amri Kumi] kwa imani hiyo? Hasha! kinyume cha hayo TWAITHIBITISHA SHERIA [AMRI KUMI]." Warumi 3:31.

Je! hivi Biblia inajikanusha yenyewe? Je! kitu fulani kinaweza kutoweka na wakati uo huo kuthibitishwa [kuimarishwa]? Je! iliwezekana kwa mwandishi yule yule mmoja kusema mambo yanayogongana kuihusu Sheria [Amri Kumi] ile ile? Ili tuweze hasa kuwa na hakika kwamba Paulo alikuwa hasemi kwamba Agano la Kale [Mapatano ya Kale] lilikuwa ni ile Sheria [Amri Kumi], hebu na tuweke maneno haya "Agano la Kale" badala ya neno "Sheria" katika Warumi 3:31. "Basi, je! twalibatilisha Agano la Kale kwa imani hiyo? Hasha! kinyume cha hayo twalithibitisha [twaliimarisha]." Maneno hayo hayaonekani kuwa yako sawa, au sivyo? Twajua kwamba Agano la Kale [Mapatano ya Kale] lilitoweka, wala lisingeweza kuongelewa habari zake kwa njia kama hiyo. Basi, kwa wazi sana sisi tunaweza kuona ya kuwa lile agano lililofikia mwisho wake lisingteweza kuwa zile Amri Kumi.

## Agano la Kale Lilikuwa ni Kitu Gani?

Baada ya kugundua kile ambacho Agano la Kale halikuwa, sasa tuko tayari kulitambulisha kwa kuonyesha tofauti yake toka katika Neno la Mungu. Kufanya hivyo yatupasa kurudi nyuma katika Biblia hadi katika kitabu kile cha Kutoka. Watu wengi wameshindwa kuona kwamba palikuwa na zaidi ya agano moja lililohusika pale Mlimani Sinai. Mungu alimwita Musa kupanda juu ya mlima ule *kabla* ya kutoa Sheria yake [Amri Kumi], na kupendekeza agano [mapatano] kati yake na watu wake. "Musa akapanda kwa Mungu, na BWANA akamwita toka mlima ule, akisema, Utawaambia nyumba ya Yakobo, na kuwaarifu wana wa Israeli,… *ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu*; maana dunia yote pia ni mali yangu, *nanyi mtakuwa kwangu … TAIFA TAKATIFU*. Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli." Kutoka 19:3-6.

Angalia jinsi Mungu alivyomwagiza Musa kuwaeleza watu wale ahadi yake. Hapa kuna vipengele vyote vya agano la kweli. Masharti na ahadi zimewekwa kwa pande zote mbili. Kama wana wa Israeli wanalikubali pendekezo lake, basi, agano litawekwa. Je, wao waliitikiaje ahadi ile aliyotoa kwao Mungu? "Musa akaenda akawaambia wazee wa watu, akawafunulia maneno hayo yote, BWANA aliyokuwa amemwagiza. *Watu wote* wakaitika pamoja wakasema, *Hayo yote aliyoyasema BWANA tutayatenda*. Naye Musa akamwambia BWANA maneno ya hao watu." Kutoka 19:7,8.

Mara tu jibu lile lilipomfikia Mungu, msingi wa Agano la Kale [Mapatano ya Kale] ukawa umewekwa. Lakini kabla ya [Agano la Kale] kuanza rasmi kazi yake palikuwa hapana budi kuwapo shughuli ya kuyatia muhuri au kuyathibitisha mapatano yale. Huduma hiyo ya matambiko ilihitaji kunyunyiza damu ya ng'ombe juu ya watu wale, nayo imeelezwa katika Kutoka 24:4-8. "Basi Musa akayaandika maneno yote ya BWANA, akaondoka asubuhi na mapema, akajenga madhabahu chini ya mlima, na nguzo kumi na mbili, kwa hesabu ya kabila kumi na mbili za Israeli, akapeleka vijana wa wana wa Israeli, waliotoa sadaka za kuteketezwa … za amani za ng'ombe. Musa akatwaa nusu ya ile damu, akaitia katika mabakuli; na nusu ya ile damu akainyunyiza juu ya madhabahu. Kisha akakitwaa kitabu cha agano [mapatano] akakisoma masikioni mwa watu, akasema, *Hii ndiyo damu ya agano* [mapatano] *alilolifanya BWANA pamoja nanyi katika maneno haya yote.*"

Tunakumbushwa tena kwamba agano hilo [mapatano hayo] halikuwa ile Sheria yenyewe [Amri Kumi], bali lilifanywa "katika maneno haya yote." Amri Kumi zilikuwa *msingi wa mapatano* yale. Watu waliahidi kuishika Sheria ile [Amri Kumi] na Mungu naye kwa upande wake aliahidi

kuwabariki. Udhaifu mkubwa sana katika mpango ule wote ulitegemea namna walivyoahidi wale Israeli. Hapakuwa na pendekezo lo lote kwamba wasingeweza kutekeleza kikamilifu kila takwa la Mungu. Wala hapakuwa na ombi lo lote la kupewa msaada wa [neema ya] Mungu. "Sisi tunaweza kutenda," wakasisitiza. Hapo ndipo ulipo mfano kamili wa *kuutegemea mwili*, na *kuzitumainia nguvu za kibinadamu*. Maneno hayo yamejaa kujitumainia wenyewe. *"Hayo yote* aliyoyasema BWANA *tutayatenda*, tena *tutayatii*."

Je! hivi waliweza kuitimiza ahadi ile? Licha ya uthibitisho wao uliorudiwa tena na tena, kwa namna ya kusikitisha mno *walilivunja neno lao kabla Musa hajashuka mlimani na mbao zile za mawe* [Ebr. 8:9; Yer. 31:32]. Je, tunaanza kuona mahali zilipokuwa zile ahadi duni katika lile Agano la Kale [Mapatano ya Kale]? Kitabu cha Waebrania sasa kinaanza kueleweka. Humo tunapewa taarifa isemayo kwamba Mungu "awalaumupo." Waebrania 8:8. Yeye alisema, "Kwa sababu hawakudumu katika agano langu [mapatano yangu] … Mimi nami sikuwajali." Fungu la 9. Lawama inawekwa kwa haki upande wa kibinadamu katika mapatano yale ya pande mbili. Hivyo tunaweza kuona barabara kwa nini Paulo aliandika kama vile alivyoandika juu ya hilo Agano la Kale katika Waebrania 8. Lilileta utumwa, lilionekana kuwa na upungufu, lilikuwa na ahadi hafifu, kisha lilitoweka - hayo yote ni kwa sababu wale watu walishindwa kutii sehemu yao iliyowahusu katika mapatano yale. Tukiyaweka pamoja mambo yote hayo, tunaweza kuona kwa nini Agano Jipya [Mapatano Mapya] lilihitajika vibaya sana, ambalo lingekuwa na ahadi zilizo bora.

Zilikuwaje bora ahadi za Agano Jipya [Mapatano Mapya]? *Kwa sababu ni Mungu aliyezitoa, tena zilihakikisha kuwapo kwa utii wenye mafanikio* [upande wa mwanadamu] *kwa nguvu zake* [Mungu] *peke yake.* "Nitawapa Sheria zangu [Amri Kumi] katika nia zao … Nami nitakuwa Mungu kwao … Nitawasamehe maovu yao, na dhambi zao sitazikumbuka tena." Waebrania 8:10-12.

Lilithibitishwaje lile Agano Jipya [Mapatano Mapya]? Kwa njia ile ile lilivyothibitishwa lile la Kale - kwa kumwaga damu yake, yule Mwana wa Mungu asiye na dhambi angeweza kutoa ile *damu ya kunyunyiza*. "Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, *kwa damu ya Agano la Milele*, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake; naye akifanya ndani yenu lipendezalo ndani yake, kwa Yesu Kristo." Waebrania 13:20,21.

Ni tofauti ilioje ukilinganisha na ahadi zile dhaifu zilizofanywa na Israeli pale Sinai kwa kutegemea mwili. Badala ya maneno yale ya watu waliyosema "tutayatenda," ahadi ya Mungu ya Agano Jipya [Mapatano Mapya] ni ku"wafany[a] ninyi kuwa *wakamilifu katika kila tendo jema* … akifanya ndani yenu." Sio tena kwa juhudi ya kibinadamu peke yake. Wala si ninyi mfanyao, bali ni yeye "akifanya kazi ndani yenu." Je, uwezo huo unapatikanaje? "Kwa damu ya *Agano la Milele*." Kutokana na kile alichofanya Yesu pale msalabani.

### Dhana Mpya Imejengwa juu ya Kuongoka

Hilo linatuleta sisi kwenye kiini hasa cha utendaji wa Agano Jipya [Mapatano Mapya]. *Utii unawezekana kwa kuandikwa Sheria ya Mungu* [Amri Kumi] *moyoni*. Kwa *kuzaliwa upya kiroho nia na moyo hubadilika.* Kristo anaingia hasa katika maisha ya mmumini na *kumpa nguvu zake mwenyewe* ili *apate kutii*. Kwa kushiriki tabia ile ya uungu mwanadamu aliye dhaifu kuliko wote *anaanza kuishi maisha yale yale hasa ya Yesu Kristo*, akiudhihirisha ushindi wake [Kristo], na kuusulibisha mwili wake.

Paulo analielezea tendo hilo kwa maneno haya: "Maana yale yasiyowezekana kwa Sheria [Amri Kumi], kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, *aliihukumu dhambi*

*katika mwili; ili maagizo ya torati* [Amri Kumi] *yatimizwe ndani yetu sisi,* tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." Warumi 8:3,4.

Neno lenye maana ya *haki* (righteousness) ni "*dikaima,*" likimaanisha "takwa la haki" la sheria. Kwa maneno mengine, kwa sababu ya maisha ya Yesu yasiyokuwa na dhambi aliyoishi katika mwili, basi, matakwa ya Sheria [Amri Kumi] yanaweza kutimizwa ndani yetu. Aliishinda dhambi katika mwili unaofanana na huu tulio nao sisi, ili aweze kutupatia ule ushindi wake. Maisha yake matakatifu ya kujitenga mbali na dhambi, yeye ataweza kabisa kuishi ndani ya miili yetu hii ya udongo, kama tukimruhusu kufanya hivyo. Hii ndiyo ahadi ya Agano Jipya kwa kila mtoto wa Mungu aaminiye na kumtegemea yeye. Ni njia pekee ambayo kwayo mtu awaye yote anaweza kutimiza kabisa matakwa ya hiyo Sheria [Amri Kumi]. "Kristo ndani yetu, tumaini la utukufu." Wakolosai 1:27. "Na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20.

Ni jambo la maana sana kwetu sisi kujua kwamba Sheria ya Agano Jipya [Mapatano Mapya] iliyoandikwa moyoni ni Sheria ile ile kabisa iliyokuwa imeandikwa juu ya mawe yale [Amri Kumi]. Kanuni zile kuu za kiroho zinaakisi [zinaonyesha] tabia halisi ya Mungu, na hizo ndizo *msingi wa serikali yake.* Tofauti haimo katika Sheria hiyo [Amri Kumi], bali katika *utendaji* wa Sheria hiyo. Zikiwa zimeandikwa tu juu ya mbao zile za mawe, zinaweza kutushtaki na kutuletea mauti tu kwa kuwa "nia ya mwili … *haitii Sheria ya Mungu* [Amri Kumi]." Warumi 8:7. Ikipokewa ndani ya moyo ambao umefanywa kuwa wa kiroho kwa neema yake Kristo iongoayo, basi, Sheria iyo hiyo [Amri Kumi] hugeuka na kuwa furaha. Mpendwa Yohana alitangaza, alisema: "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, *kwamba tuzishike amri zake* [kumi]; wala amri zake [kumi] si nzito." 1 Yohana 5:3. Sio tu kwamba Sheria hiyo [ya Amri Kumi] si nzito kwa mtoto wa Mungu aliyejazwa Roho, bali utii unaotolewa kwa furaha unawezekana kwake. Mtunga Zaburi aliandika, alisema, "Kuyafanya mapenzi yako [Kuzishika Amri zako Kumi], Ee Mungu wangu, *ndiyo furaha yangu*; Naam, Sheria yako imo [Amri zako Kumi zimo] moyoni mwangu." Zaburi 40:8.

## Hakuna Badiliko Lililofanywa Katika Agano Jipya Baada ya Kalvari

Kwa kuwa Agano Jipya [Mapatano Mapya] lilithibitishwa kwa damu yake Kristo, ni wazi kwamba lisingeanza kazi yake mpaka baada ya Yesu kufa pale msalabani. Ukweli huu wa maana sana ni lazima usipuuziwe. Uzima wa milele au mauti hutegemea juu ya ufahamu sahihi wa pointi hii ambayo ni ufunguo wake. Paulo aliandika hivi: "Maana agano la urithi lilipo, *lazima iwepo mauti yake aliyelifanya*. Kwa maana agano la urithi *lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu*; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya." Waebrania 9:16,17. Neno hili "agano la urithi" (testament) ni neno lenye maana sawa na "agano" (covenant). Ni baada tu ya wosia wa mwisho wa mtu na agano la urithi linapokuwa limethibitishwa kwa kifo chake ndipo mafao yaliyomo mle yanaweza kutekelezwa. Vile vile agano lake Kristo au agano lake la urithi lingeanza kufanya kazi yake mara tu alipokuwa amelithibitisha agano lile kwa kifo chake pale Kalvari.

Fungu lingine haliachi shaka lo lote juu ya hoja hii: "Ndugu zangu, nanena kwa jinsi ya kibinadamu. Lijapokuwa ni agano la mwanadamu, hata hivyo *likiisha kuthibitika*, *hakuna mtu alibatilishaye*, *wala kuliongeza neno*." Wagalatia 3:15. Hapa Paulo anasema kwamba baada ya kifo cha mtu wosia wake au agano lake *haliwezi kubadilika.* Hakuna nyongeza mpya hata moja iwezayo kufanywa baada ya kifo cha yule aliyelifanya. Agano hilo husimama milele sawasawa kabisa na vile lilivyosimama wakati alipokufa yule mwenye kulifanya. Baada ya kifo chake Kristo, hakuna badiliko lo lote ambalo lingeweza kufanywa katika mapatano yake ya kumwokoa mwanadamu. Masharti yote

yalitiwa muhuri na kuthibitishwa kwa kumwagwa damu yake. Kila takwa lilikuwa limewekwa wazi kwa kiolezo [mfano] kikamilifu cha maisha yake yasiyokuwa na dhambi [yasiyokwenda kinyume na Amri Kumi], na mapatano yalikuwa yamefanywa ya kuandikwa kwa Sheria yake iliyotukuzwa [Amri Kumi] na Roho Mtakatifu katika nia ya kila muumini.

Chini ya masharti ya lile Agano Jipya [Mapatano Mapya] asingeachwa peke yake mtu hata mmoja kupigana na tamaa zenye nguvu za tabia yake ya asili iliyoanguka bila kupewa msaada wo wote [na Mungu]. "Na dhambi ilipozidi, *neema* ilikuwa nyingi zaidi." Warumi 5:20. Ahadi zile za milele zenye msingi wake katika tabia ya Mungu isiyobadilika kamwe zingeweza kutoa uwezo wa kushinda kila udhaifu uliorithiwa na ule uliopatikana kwa kujizoeza. Si ajabu, basi, kwamba Biblia inazitilia mkazo "*ahadi zilizo bora*" za mapatano haya mapya yenye utukufu!

Basi ni rahisi kuelewa baadhi ya mambo aliyofanya Yesu kabla tu hajafa. Kwa mfano, kwa nini alianzisha Meza ya Bwana kabla ya mwili wake kuvunjwa? Usiku ule wa Alhamisi kabla ya kifo chake kichungu kutokea siku ile ya Ijumaa, Yesu alikutana na wanafunzi wake katika chumba kile orofani. Akikishika kikombe mikononi mwake, alisema, "*Hii ndiyo damu yangu ya agano* [mapatano], *imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi*." Mathayo 26:28.

Je, si jambo la ajabu kwamba Kristo aliweza kusema maneno yale kabla ya damu yake kumwagika? Alikuwa anatoa agizo la kufanya ukumbusho kwa ajili ya tukio lililokuwa bado halijatokea! Kwa nini? Kwa sababu lilipaswa kuingizwa kabla ya kifo chake ili kuwa katika Agano Jipya [Mapatano Mapya]. *Hakuna cho chote ambacho kingeweza kuongezwa baada ya kifo chake.*

Hebu sasa na turudi kwenye kisa nilichoanza kusimulia mwanzoni mwa ujumbe huu. Nilikuwa ndio kwanza nimemaliza tu kuhubiri juu ya somo la Sabato katika mmojawapo wa mikutano yangu ya injili. Nilipotoka pale jukwaani ili kuwasalimu watu walipokuwa wakiondoka, wanaume vijana watatu walizuia njia yangu iliyopita kati ya viti katika jengo lile maalum. Mmoja wao alizungumza nami kwa sauti kubwa - kubwa kiasi cha kutosha kuwafanya karibu watu hamsini hivi waliokuwa katika viti vya mbele kusimama na kusikiliza. "Ndugu Joe," alisema, "sisi tumesikitishwa usiku wa leo kwa namna ulivyotuweka chini ya Agano la Kale. Je! wewe hutambui kwamba sisi tunaishi sasa chini ya Agano Jipya, na tungepaswa kuitunza Jumapili badala ya Sabato [Jumamosi]?"

Ijapokuwa sehemu kubwa ya mkutano ule walikuwa wakitoka nje ya jengo lile, kundi lile lililokuwa limekaa katika viti vya mbele lilikusanyika na kukaribia zaid kuweza kusikia kile ambacho wanaume wale vijana walikuwa wakisema. Ilikuwa dhahiri kwamba ingenipasa kutumia muda fulani kujibu swali hilo la changamoto toka kwa wale watatu. Kama nilivyoshuku, walikuwa ni wanaseminari vijana waliokuwa mafunzoni katika Chuo cha Biblia cha mahali pale. Kwa shauku wakazishika Biblia zao mikononi mwao, na kungojea jibu langu kwa furaha kuu.

Kwa kawaida, mimi sipendi kubishana juu ya mambo yenye utata katika mikutano ya hadhara kwa kuogopa kuziamsha tabia za watu zinazopendelea kugombana, lakini ilionekana ya kwamba hapakuwa na njia ya kukwepa kushughulika pamoja na wachungaji wale wanafunzi. Kwa vyo vyote vile, walikuwa wamezuia njia yangu kabisa, na kundi lile la wasikilizaji likanitazama na kutazamia kupata maelezo ya aina fulani.

"Vema, yaonekana kana kwamba ninyi mmejifunza somo la maagano kwa kina sana," nikatoa maoni yangu.

"Naam," wakaniunga mkono, "tunajua kila kitu juu ya maagano hayo."

"Vema," nikajibu. "Bila shaka ninyi mnajua ni lini lilipoanzishwa Agano la Kale." Mmoja wao akasema kwa haraka, "Lilianzishwa katika Mlima ule wa Sinai."

"Je, lilithibitishwaje?" nikauliza. Bila kusita hata dakika moja mmoja wao akajibu, "Kwa kunyunyizwa damu ile ya ng'ombe."

"Vizuri sana," nikaeleza, "na lile Agano Jipya lilithibitishwaje?" Wote watatu kwa pamoja waakajibu, "Kwa damu ile ya Yesu pale msalabani."

Nikawasifu wanaume wale vijana kwa ujuzi wao wa Maandiko, na kuwaomba wanisomee mafungu mawili kutoka katika Biblia zao wenyewe - Waebrania 9:16,17 na Wagalatia 3:15. Waliitikia kwa shauku mwaliko ule, na kuyasoma mafungu yale, wakitoa ufafanuzi wao kwa kila moja baada ya kusoma. "Tunaafiki kwamba Agano Jipya halikuanza kutumika mpaka baada ya Kristo kufa, wala hakuna cho chote kinachoweza kuongezwa, wala kupunguzwa baada ya yeye kulithibitisha pale msalabani," akasema kwa dhati yule mnenaji wa kundi lile. Wote watatu wakainamisha vichwa vyao chini kwa nguvu juu ya pointi hiyo.

"Mimi nikasema, "Sasa hamna budi kunijibu maswali mawili zaidi. Hili ni swali la kwanza, nanyi hamna budi kufikiri kwa makini ili kunipa jibu sahihi: "Utunzaji wa Jumapili ulianza lini?" Pakawa na dakika moja ya ukimya uliojaa fadhaa, kisha dakika moja nyingine, na nyingine. Wavulana wale wakatazamana, na kisha wakatazama chini kwenye miguu yao, na halafu wakanitazama mimi tena. Kwa upole nikawachokoza ili wanipe jibu, "Hakika ninyi mnaweza kuniambia jibu la swali hili. Mmeyajua yale mengine yote, na kujibu kwa usahihi. Ni lini na kwa nini mnadhani watu walianza kuitunza Jumapili?"

Mwisho, mmoja wao, akasema, "Tunaitunza Jumapili kwa kukumbuka ufufuo wa Yesu." Nikasema, "Basi, yanipasa kuwauliza swali langu la mwisho. Je, utunzaji wa Jumapili ungewezaje kuwa sehemu ya Agano Jipya? Mmekwisha kusema sasa hivi kwamba *hakuna cho chote ambacho kingeweza kuongezwa baada ya kifo chake Kristo.* Iwapo Jumapili iliongezwa baada ya kufa Yesu, basi, isingeweza kamwe kuwa sehemu ya Agano Jipya, au sivyo?"

Wanaume vijana wale watatu wakageuza-geuza miguu yao huku na huku, wakaangalia huku na huku kama watu wasio na msaada wo wote, na mmoja wao akasema, "Tutajifunza suala hilo na kuzungumza nawe baadaye." Kisha kwa haraka kama walivyoweza wakatimua mbio kutoka katika jumba lile la mikutano. Naweza kukuhakikishia wewe pia kwamba kamwe hawakurudi kuendelea kuzungumza zaidi juu ya maagano hayo.

Ukweli ni kwamba Utunzaji wa Jumapili, hata kama ungeanza siku ile ya ufufuo, ungekuwa umechelewa kwa siku tatu na kuchelewa mno kuweza kuingia katika lile Agano Jipya [Mapatano Mapya]. Biblia na historia, vyote viwili, hututhibitishia ya kwamba *Jumapili haikutunzwa kamwe na Kanisa lile la Mitume.* Iliongezwa baadaye sana kama matokeo ya uasi ulioanza taratibu na kujitokeza katika karne zile za mwanzo, na ambao ulifikia kilele chake katika maridhiano na upagani yaliyofanywa na Konstantino (Constantine) katika mwaka ule wa 330 B.K.

Mamilioni ya washiriki wa kanisa wa siku hizi wanaiheshimu Jumapili kama siku takatifu ambayo inaweka ukumbusho wa ufufuo wake Kristo. Ni kweli kabisa kwamba Kristo alifufuka siku ile ya kwanza ya juma [Jumapili], lakini hakuna mahali po pote katika Biblia tunapoagizwa kuitunza siku hiyo kama takatifu. Matukio kama vile kusulibiwa na ufufuo yangekuwa ya maana sana kwa kila Mkristo, lakini hakuna dokezo hata moja lililotolewa katika Biblia la kuitunza Ijumaa au Jumapili. Siku pekee iliyopata kuamriwa kwa ajili ya ibada ya kila juma ni ile siku ya saba ya juma [Jumamosi] - yaani, Sabato ile ile iliyotunzwa na Mungu katika juma lile la uumbaji (Mwanzo 2:1-3) na ambayo ataitunza pamoja na watu wake katika milele zile zote (Isaya 66:22,23).

*Sababu yenye nguvu kabisa ya kuikataa ibada ya Jumapili ni kwamba HAIKUINGIZWA KATIKA MASHARTI YA AGANO JIPYA* [Mapatano Mapya] ambayo yalithibitishwa kwa kifo chake Yesu. Endapo Kristo angetaka ufufuo wake ukumbukwe kwa kuitunza Jumapili, basi, angekuwa ameianzisha usiku ule ule wa Alhamisi alipoiweka Meza ya Bwana. Hapo ndipo ingekuwa sehemu ya Agano Jipya [Mapatano Mapya], pamoja na ile huduma ya Meza ya Bwana na kutawadha miguu. Yesu hakusita kuamuru uadhimishaji wa kifo chake, hata ingawa kilikuwa hakijatokea bado. Kwa urahisi kama ule

angeweza kuamuru kuadhimisha ufufuo wake, ambao ulikuwa bado uko mbele, ili upate kuwa sharti la Agano Jipya [Mapatano Mapya]. LAKINI YEYE HAKUFANYA HIVYO! Wala hakuna ye yote mwingine aliyepata kufanya hivyo, mpaka unabii wa Paulo ulipoanza kutimia kuhusu ule uasi utakaofuata baada ya kuondoka [kufa] kwake (Matendo 20:29,30). Pia alizungumza juu ya ukengeufu [kuiacha njia ya kweli] ambao ungeishia katika kumtawaza katika kiti cha enzi yule Mpinga Kristo [Mpingamizi] (2 Wathesalonike 2:3,4). Lakini ni kweli kwamba hakuna dokezo lo lote katika Maandiko la kuwako kwa badiliko lo lote la ile Sheria [Amri Kumi]. Sheria ya Mungu [Amri Kumi] isiyobadilika kamwe ilihifadhiwa kama ufunuo kamili wa mapenzi ya Mungu katika Agano la Kale [Mapatano ya Kale] na katika Agano Jipya [Mapatano Mapya].

## Ishmaeli na Isaka
## Huwakilisha Maagano hayo Mawili

Tukiwa na msingi huo, basi, tuko tayari sasa kuchunguza Wagalatia 4. Wengi wamechanganyikiwa kutokana na mfano alioutumia Paulo kulifafanua Agano la Kale [Mapatano ya Kale] na Agano Jipya [Mapatano Mapya]. Hivi ndivyo jinsi alivyoandika kwa habari zake. "Kwa maana imeandikwa ya kuwa, Ibrahimu alikuwa na wana wawili, mmoja kwa mjakazi, na mmoja kwa mwungwana. Lakini yule wa mjakazi alizaliwa kwa *mwili*, yule wa mwungwana kwa *ahadi*. Mambo haya husemwa kwa mfano; kwa maana hawa ndio kama *maagano mawili*, moja kutoka Mlima Sinai ulioko arabuni, umelingana na Yerusalemu ya sasa; kwa kuwa unatumika [uko katika hali ya utumwa – KJV] pamoja na watoto." Mafungu kuanzia la 22 hadi 25.

Paulo anachora picha ya Isaka na Ishmaeli, wana wale wawili wa Ibrahimu, kuonyesha kwamba wanawakilisha Agano la Kale [Mapatano ya Kale] na Agano Jipya [Mapatano Mapya]. Anaonyesha dhahiri kwamba mwana wa Hajiri, Ishmaeli, ni mfano wa Agano la Kale [Mapatano ya Kale], na mwana yule wa Sara, Isaka, ni kivuli [mfano] cha Agano Jipya [Mapatano Mapya]. "Basi, ndugu zangu, *kama Isaka sisi tu watoto wa ahadi* … Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana." Mafungu kuanzia lile la 28 hadi 31.

Jambo hilo linavutia sana. Kwa jinsi gani wana wale wa wanawake wale wawili wanayawakilisha maagano hayo mawili? Kwa kweli, hicho ni kielelezo kamili kulingana na kila kitu tulichokwisha kujifunza mpaka hapa. Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu kwamba atampa mwana kupitia kwa mke wake Sara, lakini kwa kuwa alikuwa na umri wa takriban [karibu] miaka 90, hakuna ye yote kati yao aliyeamini kamba jambo hilo lingeweza kutokea. Sara alijua fika kwamba tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa [tasa], na ya kwamba alikuwa amepita sana umri ule wa kuzaa watoto. Basi, akamshauri mume wake kumtwaa Hajiri, mjakazi wake, na kuzaa naye mtoto. Ilionekana kwamba hiyo ilikuwa ndiyo njia peke yake ya kumnusuru Mungu kutokana na ahadi yake isiyowezekana. Halafu Ibrahimu akaikubali mbinu ile ya kuondoa fedheha na kuzaa mwana kupitia kwa Hajiri.

Hapo tunaona kielelezo kamili cha kanuni ya Agano la Kale [Mapatano ya Kale] isemayo "[*sisi*] tutayatenda." Ibrahimu alijaribu kuitimiza [ile ahadi] kimwili, kulingana na jitihada na mipango ya kibinadamu. Mpango ule wote ukashindwa sawa na vile ahadi za Agano la Kale [Mapatano ya Kale] zilivyoshindwa kwa hakika, kwa sababu *halikuwapo tegemeo la uweza wa Mungu*. Mungu kamwe hakupata kumtambua Ishmaeli kama ndiye mzao aliyeahidiwa.

Isaka alipozaliwa, ulikuwa ni mwujiza. Mungu aliumba kiumbe kipya kabisa toka katika tumbo la uzazi lililokuwa tasa kibiolojia. Kule kutokuwezekana kimwili kukatii uweza wa Mungu, yaani, ule uweza wa Mungu wa kuumba. Isaka anawakilisha kikamilifu kanuni ile ya *uhusiano* wa Agano Jipya [Mapatano Mapya] uliojengwa juu ya *kuzaliwa mara ya pili*, yaani, uzoefu wa kuzaliwa upya, ambao unasababisha kuwamo ndani yao wote waaminio uzima wa Mwana wa Mungu. Tumbo lile la

kawaida, la kimwili la Sara lilikuwa haliwezi kabisa kuzaa tunda liwalo lote. Vile vile, mwili wa kawaida, *mwili wa tabia ya asili* na *moyo wa mwenye dhambi* hauwezi kuzaa tunda lile la *utii* [Rum. 8:7]. Mungu alipoutumia uweza wake kuumba kiumbe kipya ndani ya Sara, lile lisilowezekana likatokea, naye akazaa mwana. Mungu anapotumia uweza wake kuumba kiumbe kipya rohoni, ndipo lile lisilowezekana hutokea tena - yaani, mwanadamu huyo anakuwa wa kiroho na mtiifu.

Isaka "hakuzaliwa kwa mwili," bali "kwa Roho." Wagalatia 4:29. Kwa kuwa mwanadamu ana tabia ya asili, tena yu "dhaifu kimwili," basi, hana uwezo wo wote wa kuipata haki ile iliyo kwa njia ya Sheria [inayopatikana kwa kuishika Sheria/Amri Kumi]. Yeye pia ni lazima *azaliwe kwa Roho*. Kila jitihada inayofanywa katika kutii kwa kufuata msingi ule wa Agano la Kale [Mapatano ya Kale] itazaa tu wana wa mjakazi [mtumwa]. Sheria hiyo [Amri Kumi] ni lazima iandikwe moyoni na Roho Mtakatifu na kutimizwa na "Kristo ndani yenu."

Mfano huo wa Hajiri na Sara huifanya pointi nyingine ya maana sana ya ile kweli kuwa wazi. Wale walio chini ya Agano la Kale [Mapatano ya Kale] *ni wale WANAOZIVUNJA AMRI* [KUMI], na wale walio chini ya Agano Jipya [Mapatano Mapya] *ni wale WANAOZISHIKA AMRI* [KUMI]. Ilikuwa ni wakati ule Ibrahimu *alipomwasi* Mungu kwa kumtwaa Hajiri, alipoitimiza kanuni ile ya Agano la Kale [Mapatano ya Kale]. Alipomwamini Mungu kuwa atampa mwana kupitia kwa Sara, alikuwa *mtiifu* kwa yale mapenzi ya Mungu, na kwa uhalali anawawakilisha Wakristo wa Agano Jipya [Mapatano Mapya]. Lakini ni mara ngapi wafafanuzi [wa Biblia] wa siku hizi huyachanganya vibaya mambo hayo ya kweli! Kama wale wahubiri vijana watatu, watu hao huwashtaki wale wanaoitunza Sheria [Amri Kumi] kuwa wako chini ya Agano la Kale [Mapatano ya Kale]. Ukweli ni kinyume chake kabisa. Sheria hiyo [Amri Kumi] haitunzwi kikweli kweli mpaka iwe imeandikwa katika moyo wa muumini *aliyebadilika kabisa tabia yake.* Hapo ndipo [Sheria hiyo] inakuwa alama ya utambulisho - yaani, *ishara ya UPENDO* - kwa wale *waliozaliwa kwa Roho*. Yesu alisema, "*MKINIPENDA*, mtazishika AMRI ZANGU [KUMI – Yn. 15:10; 14:21]." Yohana 14:15. Yohana aliandika maneno haya, "Kwa maana *huku ndiko kumpenda Mungu*, kwamba *TUZISHIKE AMRI ZAKE* [KUMI]; wala amri zake [kumi – Mt. 11:28-30] si nzito." 1 Yohana 5:3.

## Tohara ya Kweli Si ya Kimwili

Je, umepata kushangaa kwa nini Mungu alimpa Ibrahimu tohara kama ishara ya Agano la Kale? Je, hiyo haionekani kuwa ni njia ya kitoto ya kuwakilisha mapatano ya maana kama yale? Hebu fikiria juu yake kwa dakika moja hivi, na huenda jambo hilo likaanza kuleta maana nyingi sana. Mungu alimpa Ibrahimu ishara ya tohara *ili kumkumbusha jinsi alivyoshindwa kwa kuutegemea mwili wake.* Katika Maandiko yote, tohara ya kimwili inahusishwa na kuutegemea mwili. Paulo aliandika hivi, "Maana sisi tu tohara, *tumwabuduo Mungu kwa Roho, na kuona fahari juu ya Kristo Yesu,* wala hatuutumainii mwili." Wafilipi 3:3.

Paulo alikuwa akilinganisha tohara ya kweli na "ile iitwayo tohara." Kule kukata mwili hakukuwa tohara ya kweli hata kidogo. "Maana yeye si Myahudi aliye Myahudi kwa nje tu, wala tohara siyo ile ya nje tu katika mwili; bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani; na tohara ni ya moyo, katika roho, si katika andiko; ambayo sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu." Warumi 2:28,29. Angalia jinsi Paulo anavyogeuka kutoka katika mwili kwenda katika Roho. Anasema tohara ya kweli hutokea moyoni, nayo inasifu kile afanyacho Mungu, wala si kile afanyacho mwanadamu. Ni kule kuikata tabia ya asili ya mwili huu kwa njia ya *kuongoka.* Kuzaliwa upya ndiyo tohara ya kweli katika maisha ya mtu.

Maelezo yaliyo wazi kabisa hupatikana katika Waraka wa Paulo kwa Wakolosai: "Katika yeye *mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono*, kwa kuuvua mwili wa nyama, kwa *tohara ya Kristo*." Wakolosai 2:11.

Hapo ile kazi ya kiroho anayofanya Kristo moyoni mwetu inaitwa tohara. Inafanyika pasipo mikono, ikionyesha kwamba *hakuna juhudi yo yote ya mwanadamu ambayo ingeweza kulifanya tendo hilo*. Si kukata nyama ya mwili, bali ni kukata tabia ya kimwili ya dhambi kwa njia ya kumruhusu Kristo kukaa ndani yetu. Hiyo itapatikana kwa wote kwa msingi ule ule usiotofautiana hata kidogo. "Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi." Wagalatia 3:29. Wote wanaompokea Kristo huwa warithi wa ahadi zote zilizofanywa kwa Ibrahimu. Wale ambao wanaishi kweli kweli maisha yale ya tohara ya moyoni, hao ndio *Wayahudi wa kweli*.

Mtu ye yote hawezi kujisifu tena kwamba yuko katika familia sahihi kimwili. Hapana tena Myahudi wala Mmataifa, mwanaume wala mwanamke. Kukubalika kumejengwa juu ya msingi wa *imani* ya kila mtu peke yake ndani ya Kristo kama Mwokozi wake. Wala hakuna mtu ye yote awezaye kudai kwamba anao upendeleo wa pekee kwa kukata govi lake kimwili. Mambo hayo yalifanywa na watu wale waliojenga kila kitu juu ya msingi ule wa "[sisi] tutayatenda." Wao walitafuta kuhesabiwa haki pamoja na wokovu wao kwa njia ya matendo ya mwili. Mpango mpya wa Mungu kupitia kwa Kristo hautegemei matendo, bali neema kwa njia ya imani.

Je! hii ina maana kwamba matendo hayana maana tena? Kwa vile ile Sheria [Amri Kumi] haiwezi kumhesabia mtu haki, je! muumini aifutilie mbali? Fundisho hili la Maagano huthibitisha na kuondoa shaka lo lote linaloweza kuwapo na kuonyesha kwamba kule kuwapo kwa Sheria [Amri Kumi] ni kwa lazima *chini ya Agano Jipya* [Mapatano Mapya] kama kulivyokuwa kwa lazima chini ya lile la Kale [Mapatano ya Kale]. Badala ya kuandikwa juu ya mbao za mawe inaandikwa moyoni [Ebr. 8:10]. Badala ya sisi kuitimiza [kwa kutegemea nguvu zetu wenyewe], inatimizwa na Yesu ndani yetu [kwa kushirikiana naye, sio kumwachia afanye kila kitu mwenyewe – Flp. 2:12,13; Tito 2:11-14; Efe. 2:8-10]. Badala ya kuishika Sheria hiyo [Amri Kumi] kwa *lengo* la kuokolewa [Rum. 3:20; Gal. 2:16], tunaishika kwa *sababu tumeokolewa* [1 Yoh. 2:3,4,6]. Matendo yale yale ya utii yapo pale pale, lakini yapo pale kwa sababu iliyo tofauti, na kutokana na nia tofauti.

Pengine, bila kutambua, twaweza kuanza kuzitegemea desturi zetu zilizojengwa juu ya mazoezi yetu ya kiroho kuliko vile tunavyopaswa kufanya. Hakuna mfumo wo wote unaoweza kutupatia sisi sifa kwa matendo yetu tuliyotenda ambao unapaswa kuziziba njia zilizo wazi za imani, upendo, na neema. *Utii* [matendo] ukiwa mahali pake hasa ni wa lazima, tena unahitajika, lakini daima unapaswa kuwa mahali pake - yaani, unapaswa kuja baada ya neema na kuambatana na upendo [Gal. 5:6; Yak. 2:21,22,26].

---

**ANGALIA:** Maneno na mafungu yaliyo katika mabano haya [ ] yameongezwa kwa ajili ya ufafanuzi na kujifunza zaidi. Yasinukuliwe.